

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO: DOMINIKA YA 5 YA KWARESIMA A - TAREHE 22.03.2026

| | | |
|---|---|---|
| 1. | **LEO DOMINIKA 22.03.2026** | **DOMINIKA YA 5 YA KWARESIMA MWAKA A**<br>**Takaso la 3 la Wakatekumeni**<br>**Mchango wa Pili ni kwa ajili ya Ujenzi** |
| 2. | **JUMATANO 25.03.2026** | Sherehe ya Kupashwa Habari Bikira Maria ya Kuzaliwa Bwana - Wahudumu ni WAWATA |
| 3. | **IJUMAA 27.03.2026** | Njia ya Msalaba saa 10:30 jioni ikiongozwa na UKWAKATA na ikifuatiwa na Misa Takatifu. Kwa kipindi cha Kwaresma, siku za Ijumaa hakutakuwa na Misa za asubuhi.<br>Matoleo kipindi cha Kwaresma ni kwa ajili ya Kampeni ya Kwaresma |
| 4. | **JUMAMOSI 28.03.2026** | Waamini wote wanaalikwa kushiriki kufanya usafi Parokiani na kuandaa mapambo kwa ajili ya Dominika ya Matawi saa 3:00 asubuhi mara baada ya sala ya Jumuiya. Kanda na Jumuiya zihamasishe waamini kushiriki kwa wingi. **VIWAWA wanaombwa kuandaa Matawi** |
| 5. | **DOMINIKA 29.03.2026**<br><br>**MISA NI MBILI TU**<br><br>**HAKUTAKUWA NA MISA YA WATOTO WALA SUNDAY SCHOOL** | **DOMINIKA YA MATAWI YA MATESO YA BWANA MWAKA A**<br><br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt.Yohane Krisostom<br>Watangaza Neno: Aqulina Felix na Yudah Thadei<br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Rita wa Kashia<br>Watangaza Neno: Marko Willium na Fred Dominick<br>**Mchango wa pili kwa ajili ya ujenzi.** |
| 6. | **KIKAO CHA WALEZI/WALIMU** | Kutakuwa na kikao cha walezi, wahudumu na walimu wote wa UTOTO MTAKATIFU na Kamati Tendaji Dominika ijayo 29.03.2026 mara baada ya Misa ya Pili. |
| 7. | **KONGAMANO LA UTOTO MTAKATIFU TAIFA** | Baraza la Maaskofu limeandaa Kongamano la Utoto Mtakatifu kitaifa jimboni Kigoma, 18-22 Juni, **Kauli mbiu**: **Kujifunza, kujitambua – Utoto Mtakatifu na Umisionari**. Gharama ya ushiriki kila mmoja Shs. 315,000/=. Mwisho wa kulipia ni tarehe 31.03.2026. |
| 8. | **JUBILEE YA 75 YA JIMBO KUU DSM** | Mhashamu sana Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la DSM anatuarifu kwamba tarehe ya uzinduzi wa Jubilei ya miaka 75 ya Jimbo imebadilika , sasa uzinduzi utafanyika Jumamosi ya tarehe 09.05.2026 badala ya tarehe iliyokuwa imetangazwa awali. |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | **RATIBA YA UCHAGUZI VMJ DEKANIA** | Uchaguzi wa VMJ ngazi ya Dekania utafanyika kama ifuatavyo:- **Jumapili 22.03.2026 kuanzia saa 4:00 asbh - 6:30 mchana**: UWAKA, WAWATA, UKWAKATA na Karismatiki Katoliki. Wahusika ni viongozi wa Kamati Tendaji za Vyama husika ngazi ya Parokia. Viongozi wa Kamati Tendaji wa Dekania waliopo sasa kama hawakuchaguliwa tena ngazi ya Parokia watashiriki tu kupiga kura lakini siyo kuchaguliwa. Pia uchaguzi wa Kamati Tendaji ya Dekania utafanyika Jumamosi ijayo 28.03.2026 saa 4:00 asubuhi. Wahusika ni viongozi wa Kamati Tendaji za Parokia, Parokia Teule na wenyeviti wa VMJ ngazi ya Dekania. **Chaguzi zote zitafanyikia Makao Makuu ya Dekani, Parokia ya Mt. Peter Claver, Mbezi Louis kwa tarehe na muda uliopangwa.** |
| 10. | **HARAMBEE MAALUM** | Harambee maalum kukamilisha ukumbi wa Parokia na rangi jengo la Kanisa iliyofanyika 22.02.2026. Waamini ambao hawakushiriki wanaweza kutoa ahadi zao kwa viongozi wa Jumuiya au viongozi wa Kamati Tendaji Parokia. Kila Jumuiya inaombwa kuchukua fomu ya kuwasilisha taarifa kamili ya kila wiki. Wote walioahidi wanakumbushwa kukamilisha ahadi zao na mwisho ni 30.04.2026. |
| 11. | **MAHITAJI KWA WAHIJATI KIPINDI CHA PASAKA** | Waamini wote wanaalikwa kutoa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya wahitaji kwa kipindi cha Pasaka ikiwa ni sehemu ya tulichojinyima kipindi hiki cha Kwaresima. Mahitaji ni kama nguo, chakula, sabuni, n.k. Vyakula vinavyoharibika kama nyama viletwe Parokiani siku ya Jumamosi Kuu 04.04.2026 saa 4:00 asubuhi. Vitu yote vikabidhiwe ofisini kwa karani na viorodheshwe kwenye daftari. |
| 12. | **MCHANGO WA KILA MBATIZWA Tshs. 2,000** | Waamini wanakukushwa mchango wa kila Mbatizwa wa Tshs. 2,000 au zaidi kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa Mbadala - Pugu awamu ya tatu 2026. Viongozi wa kila Jumuiya wachukue fomu maalumu iliyotolewa na Jimbo ofisini kwa Karani. Mwisho wa kuwasilisha ni tarehe 31.05.2026 |
| 13. | **UBATIZO WA WATOTO** | Wale wanaotaka kubatiza watoto Pasaka tarehe 06.04.2026 siku ya Jumatatu Oktava ya Pasaka wanatakiwa kuleta fomu ya kuomba huduma. Mwisho ni Jumanne 24.03.2026 |
| 14. | **WAWATA** | WAWATA watakuwa na mafungo Kiparokia yatayofanyika hapa Parokiani Jumamosi ijayo tarehe 28.03.226 saa 3:00 asubuhi. |
| 15. | **KARISMATIKI KATOLIKI** | Karismatiki Katoliki Parokia wameandaa Mafungo ya Kwaresima Jumatano tarehe 25.03.2026 hapa Parokiani kuanzia saa 5:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri. Wote mnakaribishwa. |
| 16. | **ZAKA** | Viongozi wa Jumuiya wanaomba kuchukua Bahasha za ZAKA ofisini. Dominika ya ZAKA ya mwezi Machi 2026 itakuwa tarehe 12.04.2026. |
| 17. | **HUDUMA YA MACHO** | Kutakuwa na huduma ya kupima macho hapa Parokiani Dominika ijayo tarehe 29.03.2026 mara baada ya Misa ya kwanza - saa 7:00 mchana. Kupima ni Shs. **3,000** miwani kuanzia Shs. **15,000** nakuendelea |
| 18. | **KUAPISHWA KAMATI TENDAJI** | Viongozi wapya wa Kamati Tendaji ya Parokia wataapishwa Dominika ijayo 29.03.2026 katika Misa ya Kwanza. Baba Paroko anawaalika pia |

| | | |
|---|---|---|
| | | viongozi wote wastaafu wa Kamati Tendaji Parokia pamoja na familia zao na viongozi wa Kamati Tendaji wa Jumuiya zote kusali katika Misa ya Kwanza Dominika ijayo, ana ujumbe kwao. |
| 19. | **GAZETI LA TUMAINI LETU** | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

## MASOMO YA DOMINIKA

## DOMINIKA YA MATAWI YA MATESO YA BWANA MWAKA A - TAREHE 29.03.2026

| | |
|---|---|
| **SOMO I** | **Isa.50: 4-7** |
| **WIMBO WA KATIKATI** | **Zab. 22: 7-8, 16-17a, 18-19, 22-23** |
| **SOMO II** | **Fip.2: 6-11** |
| **SHANGILIO** | **Flp.2:8-9** |
| **INJILI** | **Mt.26: 14-27:66** |